## KIGONSERA

# Shule iliyogeuka urithi kitaifa, kivutio cha utalii



Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa na Waziri Mkuu mstaafu, Kassim Majaliwa (kushoto) ni viongozi wa nchi waliosoma katika Shule ya Sekondari Kigonsera, Mbinga mkoani Ruvuma.

**Na Albano Midelo**

MBINGA ni moja ya wilaya tano zilizopo mkoani Ruvuma, iliyojificha katika Milima ya Umatengo.

Miongoni mwa vitu ambavyo wilaya hiyo inajivunia ni uwepo wa shule kongwe inayobeba simulizi nzito ya historia, uongozi na ndoto za taifa.

Shule ya Sekondari ya Wavulana Kigonsera ilianzishwa mwaka 1938, ikiwa seminari ya kanisa Katoliki chini ya Shirika la Wabenediktini wa Peramiho.

Shule hiyo si tu taasisi ya elimu, bali pia ni urithi wa kitaifa na kivutio cha utalii wa kihistoria nchini Tanzania.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Kigonsera, Ponsiano Ngungulu anasema lengo la wakoloni kuanzisha shule hiyo lilikuwa kutoa elimu ya dini ya Kikristo, hasa Ukatoliki.

Baada ya uhuru, serikali iliona ni muhimu kuitaifisha ili kuwahudumia Watanzania wote bila ubaguzi.

Mwaka 1961, serikali ilichukua rasmi uendeshaji wa shule hiyo.

Hatua hiyo ilienda sanjari na misingi ya haki na usawa, iliasisiwa katika sera za elimu za awali za taifa ikiwemo Sera ya Elimu na Mafunzo iliyosisitiza upatikanaji wa elimu bila ubaguzi wa kidini, rangi au kabila.

Hii pia inalingana na misingi ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inayosisitiza usawa na haki ya kupata elimu kwa kila raia.

Kwa zaidi ya miongo minane sasa, Kigonsera imekuwa ikitoa elimu ya sekondari kwa wavulana pekee, ikiwa na uwezo wa kubeba wanafunzi 280 kwa wakati mmoja.

Tangu kuanzishwa kwake, shule hii imetoa jumla ya wahitimu 13,266.

Kumbukumbu za shule zinaonesha kuwa asilimia 96 ya wahitimu wake wameendelea na masomo ya juu, ajira za umma, ujasiriamali na huduma za kijamii ndani na nje ya nchi.

Hata hivyo, umaarufu wa Kigonsera haupo tu kwenye idadi ya wahitimu, bali pia upo kwenye majina makubwa ya uongozi wa taifa yaliyopita kwenye madarasa yake.

**Rais na waziri mkuu; alama za dhahabu Kigonsera**

Kigonsera imeandika historia ya kipekee kwa kuwatoa viongozi wawili wa juu kabisa nchini.

Miongoni mwa hao ni Benjamin William Mkapa aliyesoma shuleni hapo kati ya mwaka 1952 na 1953, kabla ya kuhamia Ndanda, Mtwara kuendelea na masomo.

Baadaye Mkapa alikuwa Rais wa Awamu ya Tatu wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1995–2005).

Mkapa ni kiongozi aliyesimamia mageuzi makubwa ya kiuchumi na kidemokrasia na kuacha alama ya uongozi thabiti katika historia ya nchi.

Kiongozi mwingine mkubwa katika taifa hili aliyepita na kupata elimu katika shule hiyo ni Kassim Majaliwa aliyesoma kidato cha kwanza hadi cha nne shuleni hapo na kuhitimu mwaka 1980.

Baadaye mwaka 2015 hadi 2025 Majaliwa alikuwa Waziri Mkuu wa Tanzania akihudumu katika Awamu ya Tano chini ya Rais John Magufuli na kisha katika Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Majaliwa anajulikana kwa uongozi wa karibu na wananchi, usimamizi wa maafa na msimamo wa nidhamu katika utawala wa umma.

Mwanafunzi mmoja ambaye hakutaka jina litajwe gazetini anasema:

"Tuliweza kutoa rais na waziri mkuu kutoka hapa Kigonsera, kwa nini tusitoe maradufu kesho? Hapa ndipo mbegu kubwa hupandwa hata kama ardhi ni ya kijijini."

Mkazi wa Kigonsera John Kapinga anasema: "Mkapa alipokaa hapa, hakuwa rais alikuwa kijana. Lakini macho yake yalikuwa ya mbali, kama mtu anayejua hatma yake ni kubwa kuliko uwanja wa shule."

Kwa mantiki ya urithi, uwepo wa viongozi hawa wawili umeifanya shule hiyo kuwa sehemu ya utalii wa kumbukumbu ya uongozi wa Tanzania, sawa na shule kama shule za Mzumbe, Tabora Boys na Ilboru zinavyotajwa kwa uzalishaji wa viongozi wa kitaifa.

Hata hivyo anasema Kigonsera ina simulizi ya kipekee zaidi yaani rais na waziri mkuu kutoka shule moja ya pembezoni mwa nchi.

**Majengo ya kale, ukarabati na uwekezaji wa serikali**

Majengo ya shule hiyo yaliyojengwa kwa mawe na chokaa za kikoloni, yalichakaa na kuanza kufifisha uzuri wake wa kihistoria.

Serikali kwa kutambua thamani ya urithi huu, ilitoa zaidi ya Sh milioni 930 kwa ajili ya ukarabati wa mabweni, madarasa, maktaba na nyumba za walimu.

Uwekezaji huu unaakisi malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya mwaka 2020–2025 inayosisitiza kuboresha miundombinu ya shule kongwe na kuimarisha mazingira ya elimu vijijini.

Aidha, inagusa moja kwa moja malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 yanayolenga kuzalisha rasilimaliwatu, yenye uwezo wa kuongoza uchumi wa viwanda na ushindani wa kimataifa.

Leo, Kigonsera si shule tu, bali ni makumbusho hai. Wageni wanaofika hapa hutamani kugusa kuta za mawe zilizowahi kushuhudia wanafunzi wakijadiliana kuhusu falsafa, dini, siasa na mustakabali wa Tanganyika ya wakati huo. Ni mahali pa kusimama, kutafakari na kuvutiwa.

**Elimu ya kujitegemea, uwekezaji na ubunifu**

Kama historia haitoshi, Kigonsera imejenga simulizi mpya ya mafanikio kupitia programu ya elimu ya kujitegemea iliyoanza mwaka 2012 kwa miradi mitatu.

Hadi Januari 2026, miradi imefikia 11, ikijumuisha kilimo cha mahindi, migomba na mbogamboga, ufugaji wa ng'ombe, kuku wa nyama, samaki na nyuki.

Aidha, shule ina mradi wa mashine ya kusaga nafaka na kuongeza virutubisho pamoja na ujenzi wa nyumba za watumishi.

**Miradi hii inatekelezwa** kwa kufuata misingi ya Sera ya Elimu ya Kujitegemea (ESDP 2008–2017) inayohimiza shule kuanzisha miradi ya uzalishaji ili kupunguza utegemezi wa michango ya moja kwa moja kutoka serikalini.

Kisheria, miradi ya shule inasimamiwa chini ya Sheria ya Elimu, Sura ya 353, pamoja na kanuni za usimamizi wa mali za umma za shule zinazoongozwa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Hii inamaanisha kuwa, mapato yanayotokana na miradi hutumika moja kwa moja katika maendeleo ya shule kwa uwazi na uwajibikaji.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed anasema shule hiyo imekuwa shamba darasa kwa shule nyingine.

"Shughuli hizi zinawasaidia wanafunzi, wazazi na jamii. Hata hivyo, kunahitajika pia kujengwa barabara ya lami inayoingia shuleni ili kuheshimu historia yake," anasema.

Shule, historia na safari ya taifa

Kigonsera inakumbusha kuwa, uongozi hauchipuki tu mijini, bali unaweza kuzaliwa kwenye kijiji tulivu chenye ndoto kubwa.

Ni ushahidi kwamba uwekezaji katika elimu, maadili na ubunifu huzaa matunda yanayovuka mipaka.

Leo, wanafunzi wanaosoma hapo wanatembea kwenye nyayo za Benjamin Mkapa na Kassim Majaliwa; nyayo zinazowahimiza kutazama mbali, kufanya kazi kwa bidii na kuthamini historia 'inayowabeba'.

Kama Tanzania ina maeneo ya urithi kama Olduvai Gorge, Bagamoyo na Kilwa, basi pia ina urithi wa aina yake; urithi wa uongozi uliozaliwa darasani Kigonsera.

Urithi huu lazima ulindwe, maana huenda kesho rais mwingine na waziri mkuu mwingine wakaibuka tena hapo Kigonsera.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Kigonsera.



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Ahmed Abbas (katikati) alipotembelea Shule ya Sekondari ya Kigonsera wilayani Mbinga.